TANGAZO LA SERIKALI Na. 64 la tarehe 31/1/2025

SHERIA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI,
(SURA YA 263)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 54(2))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MAPENDEKEZO YA KUBORESHA MALIPO YA FIDIA YA KILA MWEZI KWA WANUFAIKA WA MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mapendekezo ya Kuboresha Malipo ya Fidia ya Kila Mwezi kwa Wanufaika wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ya Mwaka 2025.

Kusudio la Waziri
Sura ya 263

**2**.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 54(1) cha Sheria, Waziri anakusudia kufanya maboresho ya malipo ya fidia ya kila mwezi kwa wanufaika wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

(2) Maboresho ya malipo ya fidia ya kila mwezi kwa wanufaika wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi yanayokusudiwa kufanyika yatahusisha malipo yanayoanzia tarehe 1 Julai 2024.

Uhalali wa Notisi

**3**.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku sitini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya muda ulioainishwa katika aya ndogo ya (1), mnufaika, kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kuwasilisha kwa maandishi maoni kuhusu pendekezo la kuboresha malipo ya fidia ya kila mwezi ya wanufaika wa Mfuko.

Uwasilishaji maoni

**4**. Maoni yoyote hukusu kusudio la kutangaza mapendekezo ya kuboresha malipo ya fidia ya kila mwezi kwa wanufaika wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi yanapaswa kuwasilishwa kupitia anwani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,
Mtaa wa Kazi,
Mji wa Serikali – Mtumba,
S.L.P 2890,
40411 DODOMA.
ps@kazi.go.tz

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Viwango vya Nyongeza

| Na. | Mwaka wa Tukio | Kiwango cha Nyongeza |
|---|---|---|
| | 2016-17 | 31.3% |
| | 2017-18 | 26.3% |
| | 2018-19 | 22.3% |
| | 2019-20 | 19.0% |
| | 2020-21 | 15.2% |
| | 2021-22 | 12.0% |
| | 2022-23 | 7.8% |
| | 2023-24 | 3.0% |

Dodoma
22 Januari, 2025

RIDHIWANI J. KIKWETE,
*Waziri wa Nchi,*
*Ofisi ya Waziri Mkuu,*
*Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*